

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA MBILI

23 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 23 APRILI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu

ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

148. MHESHIMIWA ROBERT CHACHA MABOTO (BUNDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha kumalizia ujenzi wa Maboma ya Shule za Msingi na Sekondari yaliyojengwa kwa nguvu za Wananchi Bunda Mjini.

149. MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani kuhakikisha Shule zote za Sekondari nchini zinajengewa Mabweni.

150. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Wodi za Watoto, Wanawake na Wanaume katika Hospitali ya Wilaya ya Kibaha utakamilika.

WIZARA YA NISHATI:

151. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini itaisha.

152. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itajenga *substation* kubwa ya umeme Mji wa Njombe ili kukidhi mahitaji ya Wawekezaji.

153. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini umeme wa REA utafikishwa katika Kata zote za Jimbo la Vunjo.

WIZARA YA MAJI:

154. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji wa Nyasigu – Lubungo Kata ya Igalula Ngome utakamilika.

155. MHESHIMIWA KAVEJURU ELIADORY FELIX (BUHIGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mradi wa *Grid* ya Maji ya Taifa kwa kutoa maji Ziwa Victoria na Tanganyika.

WIZARA YA UJENZI:

156. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa barabara kipande cha Km 5 kutoka Mbande hadi Msongola.

WIZARA YA FEDHA:

157. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, kuna mpango gani wa kuanzisha Bima ya Kilimo kwa Wakulima nchini.

WIZARA YA AFYA:

158. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itajenga Wodi za kulaza Wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

159. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Shamba lililotelekezwa na iliyokuwa Kampuni ya Tanganyika Parkers litakabidhiwa kwa Wananchi - Manyoni.

WIZARA YA KILIMO:

160. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti utaratibu wa Wafanyabiashara wanaotoka Nje ya Nchi kununua mazao nchini wakiwa na fedha taslimu.

161. MHESHIMIWA JOSEPH ANANIA TADAYO (MWANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itakamilisha upembuzi yakinifu, usanifu, usajili na ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Kigonigoni yenye hekta 2200 Wilayani Mwanga.

**162. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA
(KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo la njaa nchini linalotokana na upungufu wa mvua.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
23 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**